



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha Uchaguzi wa Mbunge wa Jimbo la Konde kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Oktoba 2021. Katika kutekeleza jukumu hilo, Tume inatangaza nafasi za kazi ili kupata watendaji watakaosimamia zoezi hilo. Nafasi hizo ni kama zifuatazo: -

**A. Msimamizi wa Uchaguzi (Nafasi moja)**

**1. Majukumu ya Msimamizi wa Uchaguzi**

- (i) Kuratibu na kusimamia shughuli za uchaguzi katika Jimbo lake.
- (ii) Kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa watendaji wa uchaguzi walio chini yake.
- (iii) Kutunza vifaa vya uchaguzi katika Jimbo husika.
- (iv) Kusimamia matumizi ya fedha za uchaguzi.
- (v) Kushirikiana na kushauriana na mratibu wa uchaguzi katika kuleta ufanisi kwenye shughuli za uchaguzi.
- (vi) Kutoa taarifa ya mwenendo wa hatua za uchaguzi kwa kuzingatia maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

**2. Sifa za Msimamizi wa Uchaguzi**

- (i) Awe raia wa Tanzania.
- (ii) Awe mtumishi wa Umma.
- (iii) Awe na shahada au stahhada ya juu au stahhada katika fani yoyote.
- (iv) Awe tayari kujituma na kuweza kufanya kazi bila ya usimamizi wa karibu.
- (v) Awe na uzoefu katika masuala ya Uchaguzi/Uandikishaji wa Wapiga Kura.
- (vi) Awe muadilifu na mwaminifu.

**B. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Ngazi ya Jimbo (Nafasi mbili)**

**1. Majukumu ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Ngazi ya Jimbo**

- (i) Kuwa kiungo kati ya Jimbo na Wilaya.
- (ii) Kusimamia shughuli zote za Uchaguzi katika Jimbo husika.
- (iii) Kumsaidia Msimamizi wa Uchaguzi katika masuala yote ya Uchaguzi.

**2. Sifa za Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Ngazi ya Jimbo**

- (i) Awe raia wa Tanzania.
- (ii) Awe ni mtumishi wa umma.
- (iii) Awe na shahada au stahada ya juu au stahada katika fani yoyote.
- (iv) Awe tayari kujituma na kuweza kufanya kazi bila ya usimamizi wa karibu.
- (v) Awe na uzoefu katika masuala ya uchaguzi/uandikishaji wa wapiga kura
- (vi) Awe muadilifu na mwaminifu.

Kila mwombaji katika nafasi husika aainishe nafasi anayoiomba na aambatishe maelezo ya taarifa binafsi (CV) akiweka jina la taasisi anayofanyia kazi na cheo chake. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 03 Septemba, 2021.

**Barua zote zielekezwe kwa:**

Mkurugenzi wa Uchaguzi,

Tume ya Taifa ya Uchaguzi,

Ofisi ya Zanzibar,

Mtaa wa Maisara,

S. L. P. 4670,

**Zanzibar.**

**NB:** Kwa urahisi maombi yanawezakupokelewa-  
**Unguja** - Ofisi ya NEC - Maisara, Unguja; na  
**Pemba** - Ofisi Ndogo ya ZEC - Chakechake, Pemba.

**Limetolewa na:**



Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**